

GRADE 3 MID TERM 3 DECEMBER 2021
KISWAHILI

1. **UFAHAMU** (Alama 10)

1. **Soma hadithi kisha ujibu maswali yafuatayo.** (alama 5)

Mwalimu wetu alitupa kazi ya ziada ya kuweka mazingira yetu kuwa safi. Mimi na rafiki zangu tulipangana siku ya Jumamosi kutembelea soko la mji wetu kwenda kufagia. Tuliondoka asubuhi saa mbili. Sisi sote tulibeba vifagio. Tulifagia soko letu na kukusanya uchafu panapostahili.

Tulihakikisha kuwa soko letu ni safi.

- a) Ni nani alipeana kazi ya ziada? _____
- b) Kazi hiyo ilikuwa gani? _____
- c) Watoto hawa walienda kufagia soko siku gani? _____
- d) Walienda saa ngapi? _____
- e) Je, watoto walitumia nini kufagia? _____

2. **Soma hadithi kisha ujibu maswali yafuatayo.** (Alama 5)

Kuku ni ndege anayefugwa nyumbani. Mimi nina kuku wawili. Ninawapenda kuku hawa kwa sababu hunipatia mayai. Kila jioni baada ya kutoka shuleni mimi huhakikisha kuku wangu wana maji na chakula cha kutosha. Pia mimi huhakikisha wana nyumba ya kulala. Kila Jumamosi mimi hufagia nyumba ya kuku wangu.

- a) Kuku hufugwa wapi? _____
- b) Kuku hutupatia nini? _____
- c) Andika njia tatu za kumtunza kuku. (alama 3)

2. **SARUFI**

(Alama 15)

1. **Tumia 'chini ya' au 'juu ya' kukamilisha sentensi.**


(alama 5)

a)



Kikombe kiko _____ meza.

b) Mpira uko _____ kiti.




c)




Kuku yuko _____ mti.

d) Ndege yuko _____ mti.



e)



Mtoto amejificha _____ kitanda.

2. **Andika kinyume cha neno lililopigiwa mstari.**

(alama 5)

a) Maria alisafisha nyumba. _____

b) Baba alijenga ua. _____

c) Watoto walifurahishwa. _____

d) Mwalimu alisimama. _____

e) Mjenzi alipanga matofali. _____

3. **Chagua jibu sahihi.**

(alama 5)

a) _____ atatutembelea kesho. (Wewe, Yeye)

b) _____ mtacheza mpira. (Nyinyi, Wao)

c) Wanafunzi _____ watasoma hesabu. (huyu, wale)

d) Wakulima _____ watapanda mbegu. (huyo, hawa)

e) Mbwa _____ amelala. (huyu, hawa)